

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.



### TAARIFA KWA UMMA

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe. Benjamini Kawe Sitta leo amezindua rasmi zoezi la ulipaji wa fidia awamu ya kwanza kwa wakazi 179 waliokamilishiwa taratibu za kihasibu na kuwasilisha nyaraka zao na akaunti zao za benki baada ya Serikali kutoa idhini ya ulipwaji wa fidia katika barabara za Makanya, Tandale-Kisiwani, Kilongawima, na Simu 2000 wanao athiriwa na mradi wa uboreshaji wa miundombinu katika jiji la Dar es Salaam (**Dar es Salaam Metropolitan Development Project**).

Utekelezaji wa mradi huu ulisimama katika baadhi ya maeneo kutokana na kukosa fedha za kulipia fidia, na sasa utaanza kutekelezwa katika maeneo hayo yaliyopata idhini kwa sasa huku ikisubiriwa idhini ya malipo katika barabara za Kilungule na Kilimani ili malipo yaweze kukamilika na miradi hiyo kutekelezwa kwa ufanisi na kwa ubora unaotakiwa katika barabara zote zinazohitaji kulipiwa fidia.

Utekelezaji wa mradi huu unafanywa kwa awamu kulingana na mpango wa manunuzi (procurement plan) uliokubaliwa kati ya Benki ya Dunia, na Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI na Halmashauri ya ambapo katika mwaka wa fedha 2016/2017 miradi iliyoanza kutekelezwa ni ya ujenzi wa barabara tano za awamu ya kwanza ambazo hazikuhitaji fidia kati ya barabara kumi na moja zinazotakiwa kujengwa ambazo ni Makumbusho-Sokoni, MMK, Nzasa, Tanesco – Soko la Samaki, na barabara ya viwandani.

Mradi huu unatekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam ukihusisha Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa za Ilala, Kinondoni, Temeke na Ubungo ukiwa na lengo la kuboresha miundombinu, na kuzijengea uwezo katika utoaji wa huduma na kuongeza mapato.


Kazi zinazofanyika katika mradi huu zinahusisha maeneo muhimu kama ujenzi wa barabara zitakazopunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam (**local Roads**), uboreshaji wa miundombinu katika makazi yasiyopangwa (**infrastructure Upgrading in unplanned Settlements**), kuboresha mifereji ya maji ya mvua (**storm**

**water drainage**), kuweka mifumo ya kisasa ya ukusanyaji wa mapato(**Revenue collection systems**), kujenga uwezo katika miradi ya ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma(PPP Study),na miradi unganishi kati ya miundombinu ya usafirishaji na matumizi ya ardhi(**Intergrated Transportation and Land use Planning**).

Mradi wa DMDP ulianza mwaka 2010 kabla ya kuanzishwa kwa Manispaa mpya ya Ubungo ambapo barabara zinazohusika ni Makumbusho –Sokoni km 1.45, MMK Km 0.9, Nzasa Km 1.2, Tanesco-Msasani soko la Samaki Km 1.67, viwandani Km 2.1, Makanya km 5.10, simu 2000 Km 0.80 Kilimani Km 1.80, Tandale- kisiwani Km 1.30, Maji chumvi- Kilungule Km 3.00 na Kilongawima Km 1.80. Kati ya barabara hizo barabara tano za Makumbusho –sokoni, MMK, Nzasa, Tanesco- Soko la Samaki na Viwandani zimishaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, Uboreshaji wa miundombinu katika maeneo yasiyopangwa unakusudia kuboresha makazi yanayokariwa na wananchi wenye kipato duni na utahusisha kata tatu za Tandale na Mwananyamala katika Manispaa ya Kinondoni na Kata ya Mburahati katika Manispaa ya Ubungo yatakuwa na miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja na vivuko, njia za waenda kwa miguu ,taa za barabarani ,vizimba vya taka ngumu na vituo vya mabasi.

Aidha Katika utekelezaji wa mradi huu Mto Sinza(mto Ng’ombe wenye urefu wa km 7.5 utajengwa ili kupunguza adha ya mafuriko wakati wa mvua katika Kata za Kijitonyama, Tandale ,Magomeni, Makumbusho na Ndugumbi katika Manispaa ya Kinondoni na Kata za Ubungo,na Sinza katika Manispaa ya Ubungo .

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe. Benjamini Kawe Sitta , ameishukuru Serikali Kuu na Benki ya Dunia kwa jitihada za kuboresha miundombinu na kukabiliana na changamoto kubwa za usafiri zinazolikabili jiji la Dar es Salaam kwa kupunguza adha ya msongamano wa magari katika barabara zetu, kuboreshwa makazi duni na kuwa makazi bora ya kuwawezesha wananchi kuishi maisha bora,na kuwa na suluhisho la majanga yatokanayo na mvua kupitia mradi wa ujenzi wa mto Ng’ombe. Hivyo amewataka wananchi wote kuiunga mkono miradi hiyo kwa kuulinda ili idumu kwa miaka mingi.



Sebastian M. Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI**

**Tarehe 03/09/2017.**